

Final apprehended domestic violence order
Crimes (Domestic and Personal Violence) Act 2007

Walaka huu si walaka wa kisheria. Lengo lake ni kukusaidia kuelewa amri ya mahakama. Lazima ufuate amri za polisi/mahakama. Ni kosa la jinai kwa kutofuata amri za polisi/mahakama.

Ni lazima ufuate amri zifuatazo hapa chini. Ni kinyume na sheria kupuuza amri hizi. Unaweza kukamatwa na polisi na kupelekwa mahakamani. Ukikutwa na hatia na mahakama, unaweza kwenda jela kwa miaka miwili na kutozwa faini ya mpaka \$5,500 (Dola elfu tano na mia tano).

Unaweza pia kushitakiwa na kupelekwa mahakamani kwa makosa mengineyo ya kijinai. Ukikutwa na hatia na mahakama kwa makosa hayo, unaweza kupewa adhabu kali zaidi.

Ni sharti uzingatie amri hizi mpaka tarehe iliyotolewa kwa amri hizi

Amri hizi zimetolewa kuwalinda watu waliotajwa katika amri hizi.

Ni lazima uzingatie amri hizi hata kama watu waliolindwa na amri hizi hawataki uzifuate ama wanakwambia si lazima uzizingatie

Amri zihusuzo tabia

1. Hutakiwi kufanya mojawapo ya mambo yaliyotajwa hapa chini kwa watu wanaolindwa na amri hizi ama yeote ambaye wana mahusiano naye ya unyumba.
 - A) Shambulio ama tishio la shambulio
 - B) Kuwafuata, kuwanyanya ama kuwafanya wawe na woga.
 - C) Kuharibu kwa makusudi ama kwa bahati mbaya mali zozote zinazomilikiwa na watu wanaolindwa na amri hizi.

Kwa mfano:

- Ni marufuku kufanya mojawapo ya yafuatayo kama mtu binafsi, ama kuititia mtu mwingine, ama kuititia njia za kielektroniki za mawasiliano (Kwa mfano simu, ujumbe wa simu, barua pepe, mtandao wa facebook ama mitandao mengineyo ya kijamii, kumfuatilia kwa GPS).
- Hutakiwi kufanya ama kusema chochote kinachoweza kumfanya mtu anayelindwa kuwa na hofu, ama kujisikia kwamba unaweza kumdhuru ama kuharibu mali zake kwa namna yoyote, ikiwa ni pamoja na mali zote zinazomilikiwa kwa ushirika.

Amri Zinazohusu Mawasiliano

2. Hautakiwi kuwasogelea watu wanaolindwa ama kuwasiliana nao kwa namna yoyote, isipokuwa kwa kuititia mwanasheria wao.



Final apprehended domestic violence order
Crimes (Domestic and Personal Violence) Act 2007

Walaka huu si walaka wa kisheria. Lengo lake ni kukusaidia kuelewa amri ya mahakama. Lazima ufuate amri za polisi/mahakama. Ni kosa la jinai kwa kutofuata amri za polisi/mahakama.

Kwa mfano:

- Ni marufuku kumsogelea ama kuwasiliana na mtu anayelindwa kama mtu binafsi ama kupitia njia za kielektronic za mawasiliano(Kwa mfano simu, ujumbe wa simu, barua pepe, mtandao wa facebook, mitandao mingineyo ya kijamii) ama njia nyinginezo, ikiwa ni pamoja na kuwaomba watu wengine kuwasiliana nao.
- Kama mtu anayelindwa akiwasiliana na wewe na ukamjibu, haijalishi ni mara ngapi wamewasiliana na wewe ama kwa shida gani, utakuwa unavunja amri hii.

3. Ni marufuku kusogelea:

- A) Shule ama sehemu yoyote ile mtu anayelindwa anaweza kwenda kwa makusudi ya kujisomea.
- B) Sehemu yoyote wanayoweza kwenda kwa malengo ya huduma za watoto.
- C) Sehemu yoyote iliyotajwa katika amri hii.

Kwa mfano:

- Hutakiwi kwenda sehemu hizo kama mtu binafsi
- Hii inamaanisha huwezi kuhudhuria hafla ya shule, tukio maalumu la shule ama usiku wazazi na walimu inayofanyika shulenii.

4. Hutakiwi kusogelea ama kuwa mionganini mwa watu wanaolindwa kwa angalau masaa 12 baada ya kunywa pombe ama kutumia madawa ya kulevyia.

Kwa mfano:

- Hutakiwi kumsogelea ama kuwa pamoja na mtu anayelindwa kwa angalau masaa 12 baada ya kunywa pombe ama kutumia madawa ya kulevyia. Kwa mfano kama umekunywa kwa mara ya mwisho saa tatu usiku, huwezi kuwasogelea, makazi yao ama maeneo yao ya kazi mpaka baada ya saa tatu asubuhi siku inayofuata. Kama mnaishi pamoja, hii ina maana kwamba unatakiwa kutafuta sehemu nyingine ya kukaa kwa masaa 12.
- Hutakiwi kunywa pombe ama kutumia madawa ya kulevyia na mtu anayelindwa.
- Inabidi ukae mbali nao hata kama wataomba usiondoke.

5. Hutakiwi kumtafuta mtu anayelindwa isipokuwa kwa amri ya mahakama.

Kwa mfano:

- Hutakiwi kujaribu na kumtafuta mtu anayelindwa kwa mawasiliano ya kielektronic (Kwa mfano, kwa simu, barua pepe, ujumbe wa simu, ama mtandao wa facebook au mitandao mingineyo ya kijamii), intaneti ama kumwulizia mtu yeyote kama anajua walipo.



Final apprehended domestic violence order
Crimes (Domestic and Personal Violence) Act 2007

Walaka huu si walaka wa kisheria. Lengo lake ni kukusaidia kuelewa amri ya mahakama. Lazima ufuate amri za polisi/mahakama. Ni kosa la jinai kwa kutofuata amri za polisi/mahakama.

Amri kuhusu sheria ya familia na Malezi

6. Hutakiwi kuwasogelea ama kuwasiliana na watu wanaolindwa kwa njia yoyote ile, isipokuwa kama mawasiliano hayo ni:
 - A) Kupitia mwanasheria
 - B) Kwa lengo la kuhuria ushauri nasaha katika kituo kinachotambulika rasmi ama kwa amri ya mahakama, usuluhishi/upatanishi ama
 - C) Kwa amri hii ama mahakama nyingine kuwasiliana na mtoto/watoto.
 - D) Kwa makubaliano ya maandishi kati yako na mzazi/wazazi kuhusu kuwasiliana na mtoto/watoto,

Au

- E) Kwa makubaliano ya maandishi kati yako na mzazi/wazazi na mtu mwenye wajibu wa kimalezi kwa mtoto/watoto kuhusu kuwasiliana na mtoto/watoto.

Amri zihusizo sehemu ambazo Hutakiwi Kwenda

Kwa mfano:

- Hutakiwi kumsogelea ama kuwasiliana na mtu anayelindwa kama mtu binafsi ama kupitia mawasiliano ya kielektroniki (Kwa mfano kwa simu, ujumbe wa simu, barua pepe, mtandao wa facebook ama mitandao mingineyo ya kijamii) ama kwa njia nyinginez, ikiwa ni pamoja na kumuomba mtu mwagine kuwasiliana nao.
- Kama mtu anayelindwa akiwasiliana na wewe na ukamjibu, haijalishi ni mara ngapi wamevasiliana na wewe ama kwa shida gani, utakuwa unavunja amri hii na unaweza kufikishwa mahakamani.
- Kama una amri ya sharia ya mahakama ama amri yoyote ya mahakama inayohusiana na ulinzi wa mtoto/watoto unatakiwa kuwasiliana na mwanasheria kama una mashaka kuhusu unachopaswa

Kwa mfano:

- **Kwa sehemu B:** Kwa mamabo yahusuyo sharia ya familia, kutambulika ina maana ya kutambulika kwa mujibu wa sharia ya familia ya mwaka 1975.
- **Kwa sehemu E:** Kwa mfano, kama wewe na mtu anayelindwa mmefanikiwa kupata mtoto/watoto lakini mtu mwagine ana majukumu la malezi kwa mtoto/watoto wenu, ni lazima upate ridhaa yao ya maandishi kuhusu kuwasiliana na mtoto/watoto. Huyo mtu mwagine anaweza kuwa mwakilishi wa Waziri wa Familia na Hudumu za jamii, mlezi wa kisheria aliyeteuliwa na amri ya mahakama ama mzazi mlezi.

7. Hutakiwi kuishi:
 - A) Anuani moja na mtu anayelindwa, ama



Final apprehended domestic violence order
Crimes (Domestic and Personal Violence) Act 2007

Walaka huu si walaka wa kisheria. Lengo lake ni kukusaidia kuelewa amri ya mahakama. Lazima ufuate amri za polisi/mahakama. Ni kosa la jinai kwa kutofuata amri za polisi/mahakama.

- B) Sehemu yoyote iliyotajwa katika amri hii.

Kwa mfano:

- Kama umekuwa ukiishi katika anuani hii na unahitaji kuchukua chochote mionganoni mwa mali zako, unaweza kuomba amri ya mahakama, ijulikanayo kama amri ya kurejeshewa mali zako ama unaweza kuwasiliana na polisi.

8. Hutakiwi kwenda:

- A) Sehemu yoyote anapoishi mtu anayelindwa, au
- B) Sehemu yoyote wanapofanya kazi
- C) Sehemu yoyote iliyotajwa katika amri hii.

Kwa mfano:

- Hutakiwi kwenda ndani ya mipaka ya maeneo hayo.
- Eneo lolote wanapofanya kazi
- Sehemu yoyote iliyotajwa katika amri hii.

9. Hutakiwi kwenda ndani ya mita zilizotajwa katika amri hii.

- A) Sehemu yoyote wanapofanya kazi
- B) Eneo lolote wanapofanya kazi
- C) Sehemu yoyote iliyotajwa katika amri hii

Kwa mfano:

- Hutakiwi kwenda ndani ya mita 100 za mipaka ya maeneo hayo.
- Kama umekuwa ukiishi ndani ya anuani hii na ungependa kuchukua chochote mionganoni mwa mali zako, unaweza kuomba amri ya mahakama ya kuchukua mali zako ama unaweza kuwasiliana na polisi.

Amri zinazohusu silaha

10. Hurukusiwi kumiliki silaha zozote za moto ama silaha zisizoruhusiwa kwa mujibu wa sheria ya silaha zilizouiliwa ya mwaka 1998

Kwa mfano:

- Unatakiwa kukabidhi silaha zako zote za moto na silaha nyinginezo zozote zisizoruhusiwa kwa mujibu wa sheria ya silaha zilizokatajwa ya mwaka 1998 kwa afisa wa polisi kama huna uhakika kuhusu silaha ambazo hutakiwi kuwa nazo.



Final apprehended domestic violence order
Crimes (Domestic and Personal Violence) Act 2007

Walaka huu si walaka wa kisheria. Lengo lake ni kukusaidia kuelewa amri ya mahakama. Lazima ufuate amri za polisi/mahakama. Ni kosa la jinai kwa kutofuata amri za polisi/mahakama.

Amri nyinginezo

11. Polisi au mahakama wanaweza kutengeneza amri nyingine maalum kwako na familia yako.

Mahusiano yaliyo mengi hayahitaji hofu, udhibiti na dhuluma. Vitendo vyako havikubaliki. Sasa unayo amri hii ambayo ni sharti uiheshimu. Amri hii inapatikana katika mfumo wa kompyuta wa kipolisi wa NSW.

Ukatali wa majumbani humwaathiri na kumwumiza kila mmoja. Watoto wanapotendewa ukatali majumbani, wanaweza kuwa wahanga wa wagonjwa ya huzuni, kuwa na woga na kuiga tabia shambulizi na wanaweza kukumbana na utata wawapo shuleni.

Hii ni nafasi kwako kufanya mabadiliko.

Kama utapenda kuongea na mtu kuhusu namna ya kudhibiti hasira na hofu na msongo, msaada unapatikana. Piga Simu:

- Men's Referral Service on 1300 766 491 huduma inayotoa msaada kwa wanaume.
- Relationships Australia on 1300 364 277 huduma za kusaidia familia.
- The Parent Line on 1300 1300 52 huduma kusaidia wazazi.

Kama hutatekeleza kama hii amri inavyotaka:

- Unaweza kupelekwa jela kwa kifungo cha mpaka miaka 2 na kulipa faini ya mpaka \$5,500.
- Unaweza kushitakiwa na kupelekwa mahakamani kwa makosa mengine ya kijinai (kwa mfano shambulizi na vitisho) ikiwa ni pamoja na kukiuka sheria hii. Ukikutwa na hatia kwa makossa haya na mahakama, unaweza kupewa adhabu kubwa zaidi ikiwa ni pamoja na kuwekwa jela kwa kipindi kirefu Zaidi.

Mara moja kabidhi silaha zote za moto na silaha nyiginezo zisizoruhusiwa kwa mujibu wa orodha ndani ya sheria ya kudhibiti silaha ya mwaka 1998 pamoja na leseni husika na vibali ulivyonavyo kwa polisi.Ukibakia na vitu hivi, unaweza kuwa unakiuka amri hii na unaweza kushitakiwa kwa makossa mengineyo ya jinai.

Kama una maswali yanayohusu amri hii, unaweza kuwasiliana na:

- Wakili
- Huduma ya sheria ya NSW kwa namba (02) 9219 5000
- Kituo cha polisi cha eneo lako na ulizi afisa mwezeshaji wa ukatali wa majumbani (kama una mtu anayelindwa)
- Upatikaji wa sheria kuititia namba 1300 888 529 au kwa kutembelea tovuti www.lawaccess.nsw.gov.au
- Huduma za kutafsiri kuititia namba 131 450 au kwa kutembelea tovuti www.tisnational.gov.au



Women's Domestic Violence Court Advocacy Services are funded by Legal Aid NSW

